# Ee Mungu, Unisikilize

## Zab 69

RDC

Eric Mwaniki, FRANCIS, S.J.








1. Kwa ajili yako ninavumilia fedheha,
   aibu imenifunika uso wangu.
   Nimekuwa mgeni kwa ndungu zangu,
   mtu aisiyejulikana kwa wana wa mama yangu.
   Maana wivu wa nyumba yako umenimaliza,
   laumu zao wanaokutukana wewe zimenipata.

2. Nami, sala yangu inakuelekea, ee Bwana,
   wakati wa neema yako.
   Ee Mungu, unisikilize kwa wema wako mkubwa,
   kwa uaminifu wako wenye kuniokoa.
   Ee Bwana, unisikilize, maana fadhili zako ni bora;
   kwa wingi wa rehema zako uniangalie.

3. Enyi wanyonge, tazameni, furahini;
   enyi mtafutao Mungu, mioyo yenu ihuishwe!
   Maana Bwana huwasikia wahitaji,
   wala hawadharau wafungwa wake.
   Mbingu na dunia zimsifu,
   bahari na vyote viendavyo ndani yake!

Jun 21, 2023